



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
WIZARA YA AFYA



**BARAZA LA WATAALAMU WA MAABARA**

Tovuti: [www.hlpc.go.tz](http://www.hlpc.go.tz)

**TANGAZO**

**ZOEZI LA KUHAKIKI TAARIFA NA KUTENGENEZA AKAUNTI ZA WATAALAM**

**KWENYE MFUMO WA USAJILI KWA NJIA YA MTANDAO. (HPRS)**

Ofisi ya Msajili Baraza la Wataalam wa Maabara inachukua nafasi hii kuwatangazia Wataalam wote kuwa kuna zoezi endelevu la kukusanya na kuhakiki taarifa kutoka kwa Wataalam wa Maabara nchini.

Zoezi hili linatekelezwa kwa awamu, kuanzia Wataalam waliosajiliwa mwaka 2021 kurudi nyuma mpaka mwaka 2010 kwa kuwapigia simu Wataalam wote wenye usajili wa kudumu (ERP & FRP) ambao walisajiliwa kabla ya mfumo wa usajili wa kielektroniki (hprs.moh.go.tz) kuanzishwa.

Baada ya uhakiki wa taarifa za usajili na malipo, Wataalam waliokidhi vigezo watatumiwa ujumbe mfupi (SMS) wenye maelekezo ya kuingia kwenye mfumo kwa ajili ya kuhuisha leseni zao. Kwa Wataalam wote wenye madeni watatumiwa control namba kwa ajili ya kufanya malipo mapema ili waweze kutengenezewa akaunti kwenye mfumo.

Wataalamu wote wenye usajili wa kudumu mnasisitizwa kutoingia kwenye mfumo kabla ya kutumiwa ujumbe mfupi (SMS) wenye maelekezo ya kuingia kwenye mfumo

**Aidha kwa Wataalam waliofanya mitihani na kufaulu kwa mwezi wa Machi na Aprili 2022 watatumiwa ujumbe mfupi (SMS) wenye maelekezo ya kuomba usajili wa kudumu mtandaoni, hivyo hawatakiwi kuingia kwenye mfumo kabla ya kutumiwa meseji kutoka Baraza.**

Upatapo tangazo hili mtaarifu na mwenzako.

Imetolewa na:  
Ofisi ya Msajili  
Baraza la Wataalam wa Maabara.

